# Habari kuhusu

# Sheria za

# **KUINGILIA KATI**

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Nini maana ya Unyanyasaji wa nyumbani? | 3 |
| Nini maana ya amri za uingiliaji kati? | 3 |
| Jinsi gani naweza kuwa chini ya uangalizi wa sheria? | 4 |
| Amri inayotolewa na polisi | 4 |
| Inatokea nini pale polisi wanapoandika na kutoa sheria? | 5 |
| Amri inayotolewa na mahakama | 5 |
| Kuhudhuria mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa maombi | 7 |
| Nini kinatokea Amri ya uingiliaji kati inapotolewa? | 8 |
| Kitu gani kinafuatiwa? | 8 |
| Kitu gani kinatokea wakati mtu mshitakiwa anapovunja sheria? | 9 |
| Vipi kuhusu Sheria ya Mahakama ya Familia? | 9 |
| Inatokea nini kama nikitaka kubadilisha amri ya uingiliaji kati? | 10 |
| Wapi pakupigia ili kupata msaada | 11 |

# Nini maana ya Unyanyasaji wa nyumbani?

Unyanyasaji wa nyumbani ni mlolongo wa tabia mbaya ya mtu mmoja dhidi ya mtu mwingine, ndani ya uhusiano wa karibu sana kama vile ndoa, unyumba, wapenzi, au ndani ya familia ikiwa ni pamoja na katika vizazi. Unyanyasaji wa majumbani unachukua aina nyingi ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kimwili na kijinsia, matusi, vitisho na uonevu, unyanyasaji wa kihisia na kijamii, unyemeleaji, kunyimwa kiuchumi, na uharibifu wa mali. Inatokea katika sehemu zote za jamii yetu, katika miaka yote na tamaduni zote.

Unyanyasaji wa majumbani wakati mwingine hujulikana kama ukatili wa majumbani, au vurugu za familia. Kwa Jina lolote linalopewa, tabia zote za matusi hazikubaliki katika jamii yetu, na baadhi ya hizo ni wazi kuwa ziko kinyume cha sheria.

Polisi ya Australia ya Kusini inatambua kuwa ukatili wa majumbani una madhara ya kuharibu kwa waathirika, watoto wao, familia na marafiki. Polisi hutoa kipaumbele juu ya ulinzi na usalama wa kunaoendelea kwa waathirika na watoto wao, na kujaribu pale inapowezekana, kushikilia yule anayehusika na unyanyasaji kuadhibishwa kwa matendo yake

Sheria ya kuingilia kati (zamani iliitwa sheria ya kuzuia vurugu) inaweza kukusaidia kukulinda wewe na familia yako kama ni mwathirika wa unyanyasaji wa majumbani. Kijitabu hiki kinaelezea nini kitatokea kama wewe ukipigia polisi juu ya kupata sheria ya kuingilia kati. Tunaimani kuwa kitajibu maswali yako, na kukusaidia kuamua kipi cha kufanya

# Nini maana ya sheria za uingiliaji kati?

Sheria ya kuingilia ni amri iliyotolewa na polisi au Mahakama, ikizuia mtu (mtuhumiwa) kuacha tabia inayoelekeana nawe(mtu kulindwa) katika njia ambayo inaweza kukusumbua, kukutishia au kukunyanyasa au ambayo inaweza kuwa na nguvu kunyanyasa. Mtu mwingine anaweza kuagizwa **kutokufanya** mambo mbalimbali, kama vile kutokuja nyumbani kwako na mahali pa kazi, kutokwenda kwenye shule ya watoto, kutokufuata au kutazama wewe, kutokupiga simu au kutuma ujumbe kwako. Mtu mwingine pia anaweza kuamuriwa **kufanya** mambo fulani, kama vile kuhama ya nje ya nyumba anayo shirikiana nawe. Sheria inaweza kufanywa mahsusi kwa ajili yenu na hali yako.

**Ni kosa kwa mtu mwingine (mtuhumiwa) kutotii utaratibu. Hii inaitwa 'kukiuka' maadili ya sheria. Unapaswa kuwaeleza polisi kama unaamini kuwa mtu huyo amekiuka utaratibu.**

# Jinsi gani naweza kuwa chini ya uangalizi wa sheria?

Sheria ya kuingilia kati inaweza kutolewa na polisi (inayoitwa sheria ya mpito ya kuingilia kati) au inaweza kutolewa na Mahakama. Katika kila kesi, lazima kunakuwa na sababu ya kutoa sheria husika. Hii ina maana kwamba polisi au Mahakama ni lazima kuwa na mtazamo kwamba utaweza kuhusishwa katika kitendo cha unyanyasaji na mtu mwingine, isipokuwa kukiwa na sheria ya kuingilia kati ya kukusaidia. Kuna mifano mingi ya nini maana ya kitendo cha dhuluma, na polisi wanaweza kukusikiliza kwa hali yako na kukuambia kama tatizo lako linafaa kimsingi kwa ajili ya utaratibu wa sheria ya kuingilia.

Kama una misingi, Polisi wataamua ama kutoa sheria ya kuingilia kati ya mpito moja kwa moja kwa mtu ambaye anahusika na unyanyasaji, au kukusaidia kufanya maombi kwa Mahakama ili itoa sheria ya kuingilia kati. Mazingira yatamua njia ambayo inafaa kutumika. Kila njia imeelezewa katika kijitabu hiki. Unatakiwa kusoma njia zote ili kujua kile unachotakiwa kufanya.

# Sheria inayotolewa na polisi

Ikiwa polisi wameitwa kuhudhuria unyanyasaji wa tukio ambapo mtu ametenda kosa la jinai (kama vile kupiga au kuvunja mali yako), au amefanya vitisho ili kutenda kosa la jinai, na mtu yupo sasa au yuko katika mahabusu ya polisi, polisi wanaweza kutoa sheria ya kuingilia kati ya mda, pamoja na kuchunguza malalamiko yaliyotolewa.

Kwanza, polisi atazungumza na wewe kujua ni nini kilichotokea. Wao watatathmini hatari ya wewe na watoto wako toka kwa mtu mwingine. Kama wanafikiri kuna sababu ya utaratibu wa sheria ya kuingilia, na kwamba sheria itasaidia kukulinda kutoka kweye unyanyasaji, wataandika sheria ya mda ya kuingilia kati mda huu. Watoto wako wanaweza kujumuishwa katika sheria hii kama wako hatarini pia

Kama sehemu ya mchakato, polisi watahitaji maelezo kutoka kwako ambayo yanaeleza kipi kilichotokea na kwa nini unahitaji sheria ya kuingilia kati. Ikiwa polisi tayari walishawahi kuchukua taarifa kutoka kwako juu ya kosa la jinai (kwa mfano kama ulishawahi kunyanyaswa), wanaweza kutumia maelezo yaleyale

Kunaweza kuwa na taarifa nyingine muhimu ambazo unapaswa kuwaeleza polisi. Kwa mfano, kama unafikiri mtu mwingine ana bunduki, hakikisha unawaambia polisi wajue kuhusu hilo. Hii ni kwa sababu, kama sheria ya kuingilia kati ikifanywa, polisi wataondoa bunduki kutoka kwenye umiliki wa wa mshitakiwa na kuitunza kwenye kituo cha polisi.

Lazima pia uwaeleza polisi kama kuna Sheria ya Kuingilia kati ya Mahakama ya Familia. Hii ni hivyo ili polisi wahakikishe kuwa malalamiko yako yanashughulikiwa pamoja na sheria ya mahakama ya familia. Kama una nakala ya Sheria ya Kuingilia kati ya Mahakama ya Familia, ni muhimu kuitoa kwa polisi.Kama huna nakala, polisi wanaweza kupata nakala kutoka Mahakama ya Sheria ya Familia.

## Inatokea nini pale polisi wanapoandika na kutoa sheria?

Mara baada ya sheria ya kuingilia kati kuandikwa, polisi watatumikia juu yule mtu mwingine (mtuhumiwa) kwa kuwapa nakala na kuwaelezea yaliyoandikwa. Mara baada ya mshtakiwa kupewa nakala ya amri ya kuingilia kati, wanahitaji kufuata sheria yoyote ambayo imeandikwa na polisi

Sheria ya polisi ya kuingilia kati inaanza kufanya kazi mara moja.

Utapewa nakala ya amri pia. Kwa ukweli, kila mtu aliyeandikikwa kama mtu wa kulindwa atapokea nakala, hivyo kama watoto wako wameandikwa,  watapata nakala au kama ni wadogo sana, utapewa nakala kwa ajili yao.

Amri inayoandikwa na polisi, pia ni wito kwa mshtakiwa kuitika mahakamani. Utabainisha wakati, tarehe na mahali kwa ajili ya kusikilizwa Mahakama. Kwa ujumla, hii hutokea ndani ya siku nane toka amri ya polisi imetolewa. Katika maeneo ya vijijini, inaweza kuchukua muda mrefu zaidi kuliko huu maana mahakama inaweza isifanyike mara kwa mara**. Hutakiwi kwenda tarehe hii ya kwanza ya mahakama.**

Katika mjadala huu, mahakimu watatathmini amri, na kama wakikubaliana na hilo, wanaweza kuthibitisha hilo (kuiweka katika nafasi ya kudumu), au kuibadilisha hiyo (mabadiliko ya hali ya amri na kuitoa upya kwa mshtakiwa), au kuirekebisha (kuifuta sheria hiyo).

Mwendesha mashitaka wa polisi au ofisa mwingine wa polisi atakujulisha kuhusu matokeo ya kesi mahakamani.

## Amri inayotolewa na mahakama

Katika mazingira mengine ambayo si ya haraka, au wakati mtu mwingine hayuko pale, unahitaji kuomba mahakama ili itoe amri ya kuingilia kati. Polisi bado watakusaidia kufanya hivyo kwa kuandaa maombi kwa niaba yako.

**Njia nyingine ya kawaida ni kwenda kwenye kituo cha polisi, ambapo polisi watasikiliza nini kilichotokea kwako na kuamua kama una misingi ya kupewa amri ya kuingilia kati.** Kama ukifanya hivyo, polisi watachukua maelezo kutoka kwako, ukielezea hali yako na kwa nini unahitaji kizuizi cha kuingilia kati.

Kutoa maelezo yako inaweza kuchukua masaa kadhaa hivyo ili kupunguza wakati huu, jaribu kuwa tayari na kujipanga mapema kama unaweza. Chukua pamoja nawe vielelezo au habari zozote unazofikiri kuwa zinaweza kusaidia yale utakayoyasema. Hii inaweza kujumuisha:

- maelezo yoyote unayoweza kuwa umefanya kuhusu kitu ambacho huyo mtu mwingine amakuwa akifanya, ikiwa ni pamoja na lini au wapi kitu hicho kilitokea
- picha zozote ua udhibitisho wowote wa uharibifu huyo mtu mwingine amefanya kwenye mali yako
- nakala ya maelezo,barua, barua pepe au jumbe za maelezo ambazo huyo mtu mwingine anaweza kuwa amekutumia
- habari za matibabu au ripoti kama umeonana na daktari
- nakala zozote za Amri ya Mahakama ya Familia inayohusiana na watoto wako.

Tena, wafahamishe polisi kama unadhani mtu mwingine ana bunduki. Kama Amri ya kuingilia kati ikifanywa, mahakama pia itaamuru kuwa bunduki iondolewe kutoka kwa mtu mwingine (mtuhumiwa).

Kama inawezekana, ni wazo nzuri ya kupanga huduma mbadala kwa ajili ya watoto wako ili kwamba wasisikie matatizo yako wakati ukitoa taarifa yako. Kuzungumza na polisi juu ya hali yako inaweza kuwa hali ya hofu kwako, na hii inaweza kugeuka na kuchanganya watoto wako. Hata hivyo, kama huna huduma nyingine mbadala, siyo mbaya kuja nao kwenye kituo cha polisi.

Mara baada ya taarifa yako kukamilika, polisi wataandaa faili ya mahakama ambayo itatumwa kwenye kitengo cha Polisi cha Sheria. Waendesha mashitaka wa polisi wataangalia kama kuna maelezo ya msingi ya kuuliza mahakama kutoa amri ya kizuizi kwa ajili yako. Kama ndivyo, polisi watatokea kwenye mahakama kwa niaba yako.

**Utatakiwa mara nyingi kuja mahakamani pamoja nao, hata hivyo polisi watazungumza kwa niaba yako.**

Kwa maombi ya mahakamani, mtu ambaye unaomba apewe amri ya kuingilia kati hatatokea mahakama kwa ajili ya maombi yako. Kama wako pale kwa sababu nyingine na hujisikii usalama, waambie afisa wa polisi au wafanyakazi wa mahakama.

# Kuhudhuria mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa maombi

Kama umefanya maombi mahakamani ukiwauliza kutoa amri ya kuingilia kati, polisi watakujulisha ni mahakama ipi ya kwenda, tarehe na wakati.

Unapaswa kufika dakika chache kabla ili uweze kupitakweye geti la usalama wa kuangaliwa na pia kujua ambayo chumba cha mahakama ambapo kesi yako itasikilizwa. Wafanyakazi katika dawati la habari wataweza kukwambia ni chumba kipi cha mahakama unahitaji kwenda.

Kama ukichelewa au huwezi kufika mahakamani, piga na uwaeleze polisi au mahakama sababu zako kabla ya mda..

Kama unahudhuria mahakama ya **mjini**, ofisa wa polisi kutoka kitengo cha Uchunguzi cha Unyanyasaji wa Familia atakutana na kuongea na wewe. Kama unahudhuria mahakama ya **vijijini**, waendesha mashtaka wa polisi watazungumza na wewe.

Kunaweza kuwa na watu wengine kadhaa mahakamani ambao pia wanaomba amri ya kuingilia kati, hivyo unaweza kuombwa kusubiri nje ya chumba cha mahakama hadi hakimu akiwa tayari kusikiliza maombi yako. Hii ni kwa ajiri ya kulinda siri yako.

Wakati hakimu yuko tayari kusikiliza maombi yako, afisa wa mahakama atakuuliza wewe kuja katika chumba cha mahakama na kukaa katika viti vya nyuma. Wakati ukisikia jina la mtu unayeomba ili amri ichukuliwe dhidi yake, kesi yako itakuwa 'imeitwa'. Huu ni utaratibu wa mahakama na ina maana kwamba hakimu yuko tayari kufikiria maombi yako.

**Unapaswa kubaki umekaa. Huhitaji kufanya kitu chochote katika hatua hii isipokuwa kuulizwa na hakimu, wafanyakazi wa mahakama au afisa wa polisi.**

Kama hakimu anahitaji kupata ufafanuzi kitu, wanaweza kuuliza wewe kusimama ndani ya boksi ya ushahidi ili uweze kuulizwa swali. Mara nyingi hata hivyo, watakuuliza tu wakati umeketi nyuma ya mahakama, na unaweza kujibu kutoka huko. Afisa wa polisi anaweza pia kuuliza swali kama wanahitaji habari zaidi. Sikiliza maswali kwa makini na uwajibu kwa ukweli. Wakati hakimu amefanya maamuzi yake, atakuambia kama amri ya kuingilia kati imetolewa na masharti yake ni yapi.

Kama ukikosa kitu au hawaelewi kitu, unaweza kuuliza mwendesha mashitaka au afisa wa polisi wa Unyanyasaji wa Familia baada ya kesi kusikilizwa na watakueleza kile kilichotokea na kujibu maswali yoyote unaweza kuwa nayo.

# Nini kinatokea Amri ya uingiliaji kati inapotolewa?

Polisi wanapotoa amri ya kuingilia kati, **inaanza kufanya kazi mara baada ya kuamuliwa** na ofisa wa polisi juu ya mtu aliyetajwa kama mshtakiwa. Baada ya mahakama kutoa amri ya kuingilia kati, ni muhimu kutambua kuwa amri ya kuingilia kati **mpaka polisi wamemkabidhi nakala wao wenyewe** (kutoa amri ya kuzuiliwa) kwa mtu mwingine (mshtakiwa). Hii inaweza kuchukua siku chake baada ya kesi kusikilizwa, japokuwa polisi watajaribu kuifanya haraka iwezekanavyo.

Kama inawezekana, usimwambie mhusika kuwa polisi watakwenda kumpa amri ya kuingilia kati maana wanaweza kwa makusudi kuepuka polisi ili amri hiyo isifanye kazi. Kama mtu ni vigumu kumpata, unaweza pia kusaidia kwa kuwaambia polisi mahali pengine ambapo wanaweza kupata mtu, kama vile anuani ya kazi zao, au maeneo ambayo wanapenda kutembelea mara kwa mara.

**Polisi watakuambia ni lini amri ya kuingilia imetolewa**, hata hivyo, kama una wasiwasi kama amri imeanza kufanya kazi, unaweza kuuliza katika kituo cha polisi kilicho karibu yako wakati wowote.

Kwa upande wa amri inayotolewa na mahakama, utapokea **nakala tatu** za amri yako ya kuingilia kati katika boksi ya barua au kutoka polisi siku chache baada ya kuhudhuria mahakamani. Ni vizuri kutunza nakala moja katika sehemu ya usalama, na nakala nyingine pamoja nawe (kwa mfano, katika begi ya mkononi au gari ), na toa nakala ya tatu kwa mtu mwingine anayeweza kuihitaji (kwa mfano, sehemu ya kazi au shuleni watoto wako wanapohudhuria). Unaweza kufanya nakala nyingi kama unahitaji.

Soma nakala yako kwa makini ili ufahamu ni nini mtu mwingine (mtuhumiwa) anaweza au hawezi kufanya (hali). Kwa njia hiyo, utajua kama mtu mwingine akifanya kitu ambacho kinavunja amri yoyote, na katika hali hiyo unapaswa kuwasiliana na polisi

# Kitu gani kinafuata?

Amri ya kuingilia kati itakuwa na tarehe ya mshitakiwa kuitika mahakama **kama hawakubaliani na maelezo** katika utaratibu wa amri ya kuingilia kati. Hii inatumika kwa amri zote zinazotolewa na polisi , na zinazotolewa na mahakama. Polisi itajaribu kurekebisha utofauti wowote na itakujulisha kama kuna kuna chochote kimebadilika katika amri kuingilia kati.

Kama mtu bado hakubaliani na amri iliyotolewa baada ya kusikilizwa mahakamani, basi kutakuwa na kesi mahakamani baadaye. Katika hatua hii, unaweza kuulizwa kuja mahakamani na unaweza kutakiwa kutoa ushahidi kama utaratibu utakuwa umevujwa. Kama wakati wowote, mtu mwingine yuko katika mahakama wakati huo huo kama wako, na hujisikii salama, basi waeleze polisi na mipango inaweza kufanywa ili kujaribu kukufanya ujisikia salama.

Ni muhimu kukumbuka kwamba amri ya kuingilia inaendelea kufanya kazi hadi muda ambapo itabadilishwa au kufutwa na mahakama. Kama una mashaka juu ya wapi mambo yalivyo, uliza polisi upate taarifa za sasa na maelezo. Ni muhimu hasa kuelewa jinsi gani amri ya kuingilia kati inafanya kazi na jinsi inavyokulinda.

## Kitu gani kinatokea wakati mtu mshitakiwa anapovunja sheria?

Kama mshitakiwa (mtuhumiwa) akivunja amri yoyote kwenye masharti, hii inaitwa uvunjaji wa masharti. Hii ni kosa la jinai na mshitakiwa anaweza kushtakiwa.

Unapaswa kuwa makini usifanye kitu chochote cha kusababisha huyo mtu mwingine akiuke utaratibu. Kwa mfano, kama mtu mwingine haruhusiwi kuwasiliana na wewe, basi usiwatembelee au kuwasiliana nao.

Kama uvunjaji wa amri ya  kuingilia kati unafanyika na mshtakiwa mbele yako au kujisikia uko hatarini, unapaswa kupiga mara moja kwa 131 444 (au 000 katika kesi ya dharura) na doria inaweza kutumwa ili ikusaidie .

Kama unafikiri kwamba uvunjaji wa amri ya kuingilia umetokea lakini hauko hatarini (kwa mfano, mtuhumiwa anakupigia simu kinyume na utaratibu wa amri), **unapaswa kuripoti hii kwenye kituo cha polisi** ili uchunguzi ufanyike

Kumbuka – Amri yako ya kuingilia kati inafanya kazi tu kama ukiamua ifanye kazi. Toa ripoti mara moja kwa uvunjaji wowote.

## Vipi kuhusu Sheria ya Mahakama ya Familia?

Kama watoto wanahusika, **inaweza kuwa muhimu kupata ushauri wa kisheria** ili kukusaidia kuamua kama unapaswa kuomba mahakama ya Familia juu ya Amri ya Mahakama ya Familia. Katika baadhi ya matukio, unaweza kuwa tayari umeshakuwa na amri katika Mahakama ya Familia.

Ni muhimu kukumbuka kwamba masharti katika **Amri ya Mahakama ya Familia ynaweza kuwa juu ya amri ya kuingilia kati ya kawaida**. Polisi wanaweza kukuelezea zaidi.

# Inatokea nini kama nikitaka kubadilisha amri ya uingiliaji kati?

Kama hali yako ikibadilika, na unataka kubadili (badili)masharti yoyote katika amri ya kuingilia kati au kufuta (kurekebisha), basi unahitaji kuwasiliana na polisi na kuwaambia sababu ya kutaka kubadilisha amri ya kuingilia kati.

• Katika maeneo ya mjini. Wasiliana na kitengo cha uchunguzi cha Unyanyasaji wa Familia.

• Katika maeneo ya vijijini, wasiliana na kituo cha polisi cha karibu.

Kusikilizwa kwa kesi kwingine na mahakama kutatakiwa kuwepo ili kubadilishwa au kufutwa kwa amri. Ni muhimu kwako kuelewa kwamba ni mahakama tu inayoweza kubadilisha au kufuta utaratibu. Amri haiwezi kubadilishwa na wewe au mtu mwingine tu kwa kukubaliana kubadilisha

Wewei na huyo mtu mwingine mutaambiwa muda na tarehe ya kusikilizwa kesi. **Unahitaji** kuhudhuria mahakamani kwa hili. Mara nyingi, huyo mtu mwingine atatakiwa pia kuhudhuria, lakini si mara zote.

**Polisi na mahakama zinatambua kwamba wakati mwingine mabadiliko yanatokea kwa faida na amri inatakiwa kubadilishwa pia. Hata hivyo, polisi pia wanatakiwa kuridhika kwamba bado utakuwa salama, na kwamba hauko unasukumwa kufanya mabadiliko ambayo yanaweza kukuongezea madhara wewe na familia yako**

**Wakati mwingine, polisi hawatakubaliana kujitokeza mahakamani kwa ajiri yako ili kurekebisha au kutoa masharti kama wanaamini hatua hii itaongeza hatari yako na familia yako katika kunyanyaswa.**

# Wapi pakupigia ili kupata msaada

Kwa hali ya hatari 000

Kwa msaada wa polisi/wahudhulie 131 444

Katika maeneo ya mjini , wasiliana na Kitengo cha Uchunguzi che Unyanyasaji wa Familia:

| | | |
|---|---|---|
| Adelaide | 8172 5890 | A/H 8172 5000 |
| Elizabeth | 8207 9381 | A/H 8207 9411 |
| Holden Hill | 8207 6150 | A/H 8207 6000 |
| Port Adelaide | 8207 6413 | A/H 8207 6444 |
| South Coast | 8392 9172 | A/H 8392 9000 |
| Sturt | 8207 4801 | A/H 8207 4700 |

Vijijini wasiliana na kituo cha polisi kilicho karibu nawe.

Kama wewe ni muathirika wa Unyanyasaji wa majumbani na Kiingereza sio lugha yako ya kwanza, na unahitaji msaada na kufafanuliwa katika kuelewa mpangilio wa amri ya kuingilia kati, tafadhali wasiliana na **Huduma ya Kusaidia Wanawake Wahamiaji [Statewide Culturally and Linguistically Diverse (CALD) Domestic Violence Service]** kwa simu **8346 9417.**

Orodha ya mashirika ambayo yanaweza kuwa ya msaada zaidi na kukusaidia wewe kama mwathirika wa migogoro ya nyumbani, inapatikana kutoka kituo cha eneo lako cha polisi.

Kijitabu hiki kimeandaliwa kama huduma kwa jamii na kimeanzishwa na Polisi ya Australia ya Kusini na wakati kila aina ua uangalifu ulizingatiwa wakati wa maandalizi, hakuna uhakika unaotolewa katika kusema au kwa maandishi juu ya usahihi, ya kisasa au ubora katika kwa lengo la habari au ushauri uliotolewa na hakuna hasara au majukumu yatakayokubaliwa na serikali ya Australia ya Kusini, wizara zake, Polisi ya Australia ya Kusini na vitengo vyake, maofisa au waajiliwa kwa hasara yoyote itakayompata mtu kutokana matokeo ya kutumia ushauri au mambo yaliyoko katika kitabu hiki.

©South Australia Police

Kijitabu cha Amri ya Kuingilia Kati chaPolisi ya Australia ya Kusini (imetolewa Mei 2012) na inalindwa na haki ya kunakiri.

Maulizo kuhusu haki ya kunakiri au matumizi ya kijitabu hiki yanakaribishwa

**South Australia Police**
**Corporate Communication Branch**
**Police Headquarters**
**GPO Box 1539**
**Adelaide 5001**